OFISI YA RAIS-TAMISEMI
HALMASHAURI YA MJI-TARIME
SHULE YA SEKONDARI NYAMISANGURA
Barua pepe:
nyamisangurasstarime@yahoo.com/nyamisangurasstarime@gmail.com

S.L.P 328,
TARIME.

KUMB. NA. NYSS/JOIN INST/VOL.A/13

TAREHE: 03/12/2021

TEL:+255784625495-Mkuu wa shule
+255620289649 – Mkuu wa shu
+255783129405-Makamu mku hule
+255758266678 - Mtaaluma

JINA LA MWANAFUNZI
……
S.L.P……
TARIME.

YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI NYAMISANGURA, KATIKA HALMASHAURI YA MJI WA TARIME, MKOA WA MARA MWAKA 2022

1.0 **Utangulizi**.

Ninafurahi kukutaarifu kwamba umechaguliwa/umepewa nafasi kujiunga kidato cha I katika shule hii mwaka 2022. Shule ya sekondari Nyamisangura ipo Tarime Mjini, umbali wa Km 1 kutoka Stendi kuu ya mabasi upande kaskazini . Usafiri wa boda boda Tsh 1,000/= au Tax Tsh 5,000/= unapatikana katika kituo cha mabasi cha Tarime Mjini.

Muhula wa masomo unaanza tarehe 17/01/2022 . Unatakiwa kuripoti shuleni kuanzia tarehe 17/01/2022; na mwisho wa kuripoti ni tarehe 24/01/2022.

2.0 Mambo muhimu ya kuzingatia

2.1 **Sare ya shule**

(a) Shati nyeupe - mikono mifupi, yenye mfuko mmoja (weka mchirizi wa kijivu katika bega upande wa kushoto).

Wavulana: Suruali ya rangi ya kaki iliyoshonwa kwa ustadi. Iwe na marinda mawili kila upande kwa mbele; iwe na mifuko miwili pembeni na mfuko mmoja nyuma upande wa kulia; iwe na pindo (turn up) mguuni, na iwe pana vya kutosha kulingana na umbo la mwanafunzi. Modo haziruhusiwi kabisa.

Wasichana: Sketi ya rangi ya kaki iliyoshonwa kwa ustadi. Iwe na marinda mawili mapana, rinda moja mbele na

rinda moja nyuma; iwe ndefu mpaka miguuni; iwe na michirizi miwili mieupe kwa mbele.

Tai ya kaki ni ya lazima kwa kila mwanafunzi.

(b) Viatu vyeusi vya ngozi vya kufunga na kamba na vyenye kutumia rangi kwa wavulana na kwa wasichana. Pia Soksi nyeupe ndefu kwa wasichana na soksi nyeusi ndefu kwa wavulana.

N.B: ukishona sare tofauti na maelekezo hayo, itakulazimu ushone upya.

(c) Rangi ya Hijabu ifanane na shati ya shule na iwe ndefu kama inavyoonekana kwenye mchoro ulioambatanishwa.

(d) **Sweta** rangi ya kijani yenye shingo la V.

(e) Nembo kwenye sare ya mwanafunzi utapata maelekezo hapa shuleni baada ya kuripoti.

(f) **Sare ya michezo** ni Track suti ya bluu bahari (light blue) yenye michirizi mieupe pembeni, Raba nyeupe, na T-shirt. Maelekezo ya T-shirt utapata hapa shuleni.

2**.2 Vifaa vya darasani**

(a) Daftari (Counter Book Q3 angalau zisipupugue 13), kalamu za kutosha, Mkebe wa hesabu (mathematical set) ,Dictionary (kamusi) ni muhimu

(b) Mahitaji mengine ya kibinadamu kama matibabu, nauli na chakula ni jukumu la Mzazi.

(c) Nakala ya Cheti Cha Kuzaliwa mwanafunzi aje nayo, pamoja na jalada (Folder file na kamba yake) kwa ajili ya kutunzia taarifa zake. (Usilete faili ya plastiki).

3.0Sheria na kanuni muhimu za Shule

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu Na.25 ya mwaka 1978 kama ilivyorekebishwa kwa sheria Na 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu. Unatakiwa kuzingatia mambo ya Msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa mara baada ya kuripoti shuleni.

(a) Heshima kwa viongozi , wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.

(b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima.

(c) Kuwahi katika kila shughuli ya shule kama zitakavyopangwa.

(d) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia maelekezo juu ya kuwepo ndani au nje ya shule wakati wote wa uanafunzi wako.

(e) Kutunza usafi wa Mwili, Mavazi na Mazingira ya Shule.
(f) Kuvaa sare ya shule wakati wote na kwa kufuata utaratibu uliowekwa kwa kila sare.
(g) Kutunza majengo,samani na mali zote za umma zilizoko shuleni.
(h) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote
(i) Kuhudhuria vipindi vyote vya masomo na kufanya kazi zote za darasani.

3.1 MAMBO AMBAYO MWANAFUNZI HARUHUSIWI KUFANYA

1. Kuvuta sigara / Bangi
2. Kufuga kucha, ndevu, na nywele ndefu zisizotunzwa katika hali ya usafi.
3. Kuvaa sare isiyo ya heshima, kubana na fupi.
4. Kugombana
5. Kuiga mitindo ya kihuni, kama vile kunyoa mitindo ya kihuni, kupaka kucha rangi, kulegeza nguo, kubana nguo, n.k.
6. Kuchubua ngozi kwa kutumia madawa.
7. Kwenda nje ya shule bila ruhusa wakati wa masomo.
8. Kutohudhuria masomo na vipindi vya masomo.
9. Kuvaa kofia, bangili na mapambo mengine yoyote.
10. Kuwa na silaha shuleni.
11. **Kuwa na simu, Kamera, Kinasa sauti, mp3/mp4 player shuleni.**
12. Wageni wa wanafunzi hawaruhusiwi kuwasiliana nao bila idhini ya uongozi wa shule/walimu.

3.2 MAKOSA YANAYOWEZA KUSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE MARA MOJA NI:

(a) Wizi
(b) Uasherati, ubakaji na ushoga
(c) Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya/mihadarati.
(d) Uvutaji Bangi.
(e) Makosa ya jinai
(f) Kupigana au kupiga
(g) Kuharibu mali ya umma kwa makusudi
(h) Kudharau bendera ya Taifa.
(i) Kuoa au kuolewa.

(j) Kupata mimba au kusababisha mimba ndani au nje ya shule.
(k) Kutoa mimba
(l) Kugoma, kuchochea mgomo na kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule au watu.
(m) Kukataa adhabu kwa makusudi
(n) Kuwa na simu au silaha shuleni.

Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

_____

_____

Mkuu wa Shule

KIAMBATANISHO A

FOMU YA MAELEZO YA MWANAFUNZI NA AHADI YAKE YA KUTOSHIRIKI KATIKA MIGOMO SHULENI

1. Jina la mwanafunzi_____ Jinsi: Me / Ke
2. Tarehe ya kuzaliwa _____ Namba ya Cheti cha kuzaliwa _____ Jina la Mama _____ Jina la Baba _____
3. Siyo Yatima/ Yatima : wazazi wote walifariki/ Baba alifariki/ Mama alifariki.
4. Jina la mzazi/ Mlezi _____ Namba ya NIDA _____
   Jinsi: Me/ Ke Mahusiano_____ Namba ya Simu _____ kazi _____ Anwani S.L.P. _____ Mahali anapoishi (Mtaa) _____
5. Mwanafunzi anapoishi : Mkoa _____ Wilaya _____ Tarafa _____ Kata _____ Mtaa _____. Umbali toka Nyumbani hadi Shuleni _____Km.
6. Maelezo Mengine kuhusu mwanafunzi. **Uraia** _____ Matatizo ya kiafya kama yapo_____
   Mazingira magumu: kuvuka Mto mkubwa/ kuvuka msitu mkubwa wenye hatari/ Umbali mkubwa mno toka nyumbani hadi shuleni/ hakuna mazingira magumu.
   Ulemavu : Kutoona(upofu)/Uoni hafifu/ Kutosikia/ Ulemavu wa viungo/ Ulemavu wa akili. Malazi : Kutwa / Bweni.

Ahadi yangu mimi (Jina la mwanafunzi)

_____

Nakubali kwa dhati kabisa nafasi niliyopewa na Taifa kujiunga na Shule hii. Naahidi kutii sheria zote na taratibu zote kama zilivyotolewa na zitakazotolewa na uongozi wa shule.

Tarehe _____ Saini ya mwanafunzi _____

Mimi Jina la mzazi/mlezi _____ nakubaliana na masharti na sheria zote za **Nyamisangura Sekondari** ambako kijana wangu amechaguliwa kujiunga.

Naahidi kwamba nitamhimiza mwanangu kufuata sheria na Taratibu zote za shule. Aidha naahidi kushirikiana na Uongozi wa shule katika malezi bora ya mwanangu ili baadaye awe raia bora wa Taifa letu.Nitafuatilia maendeleo yake ya kitaaluma na kufuata matokeo yake ya kila muhula wa masomo.Vilevile nitaitikia wito wa shule pale nitakapohitajika.

Tarehe _____ Saini ya mzazi/mlezi _____

Jina la mzazi/mlezi _____.

NYAMISANGURA SECONDARY SCHOOL
MEDICAL EXAMINATION FORM.

Name _____Age _____

Height (in cm) _____Weight _____

1. Blood cont_____(red and white)_____
2. Stool examination _____
3. Urinalysis _____
4. Syphilis and other V.D _____
5. T.B and Leprosy test _____
6. Eye test _____
7. Ear _____
8. Chest _____
9. Abdomen _____
10. Plano test (girls) _____

11. Spleen _____

Additional information e.g Physical Defects or impairments, infections, chronic or family diseases (e.g sickle cell), inability to eat certain food etc.

_____

_____

_____

_____

_____

__

I certify that the above named Student is fit/not fit to pursue Secondary Education.

Signature _____ Date _____

Designation _____

Station _____